



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



MSIMAMIZI MSAIDIZI WA UCHAGUZI

KATA YA MAHEGE - HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI

Kumb. Na. IB.191/258/03/41

Tarehe 01 Julai, 2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA.

Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi Kata ya Mahege, kwa kuzingatia kanuni ya 12 na 13 za Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, anakaribisha maombi kutoka kwa Watanzania wenyewe sifa na uwezo wa kujaza nafasi za Watendaji wa Vituo vya Kupigia Kura kwa ajili ya Uchaguzi Mdogo utakaofanyika tarehe 13 Julai, 2023 katika Kata ya Mahege kama ifuatavyo: -

1. Msimamizi wa Kituo cha Kupigia Kura (Nafasi 13).
2. Msimamizi Msaidizi wa Kituo cha Kupigia Kura (Nafasi 26).
3. Karani Mwongozaji Wapiga Kura (Nafasi 13).

A. SIFA ZA WAOMBAJI WA NAFASI YA MSIMAMIZI AU MSIMAMIZI MSAIDIZI WA KITUO CHA KUPIGIA KURA.

- (a) awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;
- (b) asiwe shabiki au kiongozi wa chama cha siasa;
- (c) awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu;
- (d) awe amemaliza elimu ya kidato cha nne (4) au zaidi na anaweza kusoma na kuandika vizuri. Pia, anayeweza kusoma na kuelewa kitabu cha Maelekezo ya Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura; na
- (e) awe mkazi wa kata ambayo anaomba kufanya kazi.

B. SIFA ZA WAOMBAJI WA NAFASI YA KARANI MWONGOZAJI WA WAPIGA KURA

- (a) awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;
- (b) awe mkazi wa kata ambayo atafanya kazi ya kuongoza wapiga kura;
- (c) ikiwezekana awe mpiga kura wa kituo atakachofanya kazi;
- (d) awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu;
- (e) awe na elimu isiyopungua kidato cha nne na anayeweza kusoma na kuelewa kitabu cha Maelekezo kwa Makarani Waongozaji Wapiga Kura; na
- (f) asiwe shabiki au kiongozi wa chama cha siasa.

C. MALIPO

Malipo yatakuwa kama ifuatavyo: -

- i. Siku ya Uchaguzi Msimamizi wa Kituo atalipwa posho ya Shilingi 60,000 kwa siku kwa muda wa siku mbili, posho ya chakula Shilingi 10,000 kwa siku moja na nauli Shilingi 20,000.
- ii. Msimamizi Msaidizi wa Kituo atalipwa posho ya Shilingi 50,000 kwa siku kwa muda wa siku mbili, posho ya chakula Shilingi 10,000 kwa siku moja na nauli Shilingi 20,000.
- iii. Karani Mwongozaji Wapiga Kura atalipwa posho ya Shilingi 50,000 kwa siku moja na posho ya chakula Shilingi 10,000.
- iv. Wakati wa mafunzo Wasimamizi na Wasimamizi wasaidizi watalipwa posho ya Shilingi 50,000 na nauli Shillingi 20,000 kwa siku mbili za mafunzo, na Makarani waongozaji watalipwa posho ya Shilingi 50,000 na nauli Shillingi 20,000 kwa siku moja ya mafunzo.

D. MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE


- i. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) wawili.
- ii. Maombi yote yaambatishwe na vyeti vya taaluma, nakala ya vyeti vya kidato cha nne, kidato cha sita au kuhitimu mafunzo kwa kuzingatia sifa alizonazo kwa mujibu wa Tangazo hili.
- iii. Waombaji waambatishe picha mbili zenyе ukubwa sawa na picha iliyopo kwenye pasi ya kusafiria (Passport size) za hivi karibuni.
- iv. Waombaji ambao ni Watumishi wa Umma wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa waajiri wao.
- v. Waombaji watakaowasilisha taarifa na sifa za kugushi watachukuliwa hatua za kisheria endapo watabainika.

Maombi yawasilihwe Ofisi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi Kata ya Mahege, Mwisho wa kutuma na kupokea maombi ya kazi ni tarehe 05 Julai, 2023.

Anuani ya kutuma maombi ya kazi ni:

Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi,
Kata ya Mahege,
S. L. P 33,
KIBITI.

Limetolewa na:-



**MSIMAMIZI MSAIDIZI WA UCHAGUZI
KATA YA MAHEGE.**